

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

08 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 08 JUNI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kuhusu:

Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023; na

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 [*The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023*].

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa

Mwaka 2023 [*The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023*];

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu:

Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023;

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 [*The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023*]; na

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 [*The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023*].

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

558. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga nyumba za Walimu Shule za Msingi katika Kata za Salale, Kiongoroni, Mbuchi na Maparoni Kibiti.

559. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuchukua hatua kwa Watumishi wanaoripoti na kuondoka bila kufanya kazi Wilayani Tunduru.

560. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuwapatia vyombo vya usafiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kufuatilia mikopo inayotolewa na Halmashauri.

561. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro itakuwa Jiji.

562. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inawasaidiaje Wanafunzi wenye mahitaji maalum katika huduma za vyoo kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

563. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Kituo cha Utalii Kihesa Kilolo chini ya Mradi wa *Regrow* kitaanza kujengwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

564. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ajali ngapi za barabarani zimetokea kati ya Mikumi na Ruaha Mbuyuni kwa Mwaka 2010 hadi 2022.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

565. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itapitia Mtaala wa Vyuo Vikuu ili kufungamanisha elimu sambamba na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

WIZARA YA KILIMO:

566. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Kata ya Ikweha uliopo Jimbo la Mufindi Kaskazini utakamilika.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***[Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima
na Kusomwa Mara ya Tatu]***

Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *[The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023]*.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 *[The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023]*.

**DODOMA
08 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**